

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA**



**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU UZALISHAJI NA**  
**UPATIKANAJI WA SUKARI NCHINI**

Serikali kwa kuzingatia makubaliano yaliyofikiwa katika mkutano wa wadau wa zao la sukari uliofanyika Morogoro tarehe 8 Januari 2014, inatangaza rasmi kusitisha utaratibu uliozoeleka wa kuruhusu uingizaji wa sukari kutoka nje ya nchi, kuziba pengo kati ya uzalishaji na mahitaji (gap sugar) katika msimu wa uzalishaji unaoishia mwezi Machi 2014.

Hatua hiyo ya Serikali inakusudia kutoa nafasi kwa sukari iliyopo na inayotarajiwa kuzalishwa na viwanda vya hapa nchini kupata soko la uhakika. Aidha, hatua hiyo inalenga kuboresha kipato cha wazalishaji wa sukari pamoja na wakulima wa miwa, bila kuathiri bei na upatikanaji wa sukari hapa nchini.

Uzalishaji wa wastani wa sukari kwa mwaka hapa nchini ni tani 300,000 ambapo katika msimu wa 2013/2014 jumla ya tani 308,000 za sukari zitazalishwa. Aidha, kuna takriban tani 80,000 ya sukari imehifadhiwa katika maghala ya wafanyabiashara wa sukari hapa nchini. Kutokana na hali hiyo, nchi itakuwa na sukari ya kutosha kati ya kipindi cha sasa hadi msimu mwingine wa uzalishaji. Hivyo hakutakuwa na sukari itakayoingizwa nchini kwa lengo la kufidia upungufu kama ambavyo huwa inafanyika katika miaka mingine yenye

upungufu. Kwa ujumla mahitaji ya sukari nchini kwa matumizi ya majumbani na viwandani ni tani 590,000 kwa mwaka.

Katika kufanikisha usimamizi na utekelezaji wa agizo hilo, Serikali kupitia Mamlaka na Vyombo vyake vya udhibiti itachukua hatua zifuatazo:-

- (i) Kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Sekta ya Sukari ya mwaka 2001 ili kuhakikisha kuwa utaratibu mzima wa uingizaji sukari nchini unazingatiwa.
- (ii) Kuimarisha udhibiti wa sukari inayoingizwa nchini kwa njia ya magendo pamoja na kuhakikisha kuwa sukari inayoagizwa na nchi jirani kupitia bandari zetu (*transit sugar*) haipenyezwi kuuzwa katika soko la hapa nchini.
- (iii) Kusimamia mfumo mzima wa usambazaji wa sukari nchini ikiwa ni pamoja na kuwadhibiti wafanyabiashara wenye tabia ya kuhodhi soko la sukari kwa lengo la kusababisha upungufu usio halisi wa sukari (*artificial shortage*).
- (iv) Kuendelea kuhamasisha uwekezaji ili kuongeza uzalishaji wa ndani utakaotosheleza mahitaji na kupata ziada.
- (v) Kuweka utaratibu kwa wafanyabiashara ili itakapobidi waweze kuagiza sukari kwa jumla (*bulk procurement*) au kwa njia ya zabuni maalumu kama ilivyo kwenye sekta nyingine kama ya mafuta.
- (vi) Mapendekezo ya kitaalamu ya Kamati ya Ufundi ya Uagizaji Sukari toka nje ya nchi (*Technical Committee on Sugar Importation*) yatazingatiwa wakati wa kufikia maamuzi ya kutoa vibali kwa wafanyabiashara kuingiza sukari nchini.

- (vii) Kuweka mfumo wa kodi ya forodha ya sukari inayoingizwa nchini kutoka nje ambao utawianisha gharama za uzalishaji wa sukari inayozalishwa na viwanda vya ndani.
- (viii) Kuendelea kuhamasisha na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa wazalishaji wa sukari wa ndani ya nchi ikiwa ni pamoja na kuwa na maabara huru ya kupima kiwango cha sukari na kupunguza tozo za miwa kwa wakulima.
- (ix) Kuhakiki mahitaji ya sukari ya viwandani kwa lengo la kudhibiti uagizaji na kuhimiza uzalishaji wa aina hiyo ya sukari hapa nchini.

ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA (Mb)  
**WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA**